

## Maswali

1. Adamu alitengenezwa namna gani?
2. Hawa alitengenezwa namna gani?
3. Adamu na Hawa waliishi wapi?
4. Mungu alisema wasifanye nini?
5. Ni mti gani walikatazwa wasile?
6. Nyoka alimwambia Hawa nini?
7. Adhabu ya nyoka ilikuwa nini?
8. Adhabu ya Hawa ilikuwa nini?
9. Adhabu ya Adamu ilikuwa nini?
10. Mwokozi yupi Mungu aliwaaidi?

## Majibu

1. Adamu alitengenezwa kutoka kwa mavumbi ya nchi.
2. Hawa alitengenezwa kutoka kwa ubavu wa Adamu
3. Adamu na Hawa waliishi katika Bustani ya Edeni.
4. Mungu alisema ni sharti wasile tunda la mti ulio katikati ya Bustani.
5. Mti huo uliitwa mti wa ujuzi wa mema na mabaya.
6. Nyoka alikuwa amemwambia Hawa hautakufa.
7. Adhabu ya nyoka ni kutambaa kwa tumbo.
8. Adhabu ya Hawa ni kuwa na watoto wengi, awe mzee na afe.
9. Adhabu ya Adamu ni kufanya kazi kwa nguvu awe mzee na afe.
10. Mwokozi walioaidiwa na Mungu ni Yesu Kristo.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 1 Mwaka wa 1



## 2 Adamu na Hawa

### Marejeo

Mwanzo 3

### Kiini cha somo

Kuonyesha vile dhambi ilingia ulimwenguni kwa ajili ya kuasi, na jinsi ilivyo muhimu kutii Mungu.

### Maneno maalum

1. Adamu akaumbwa + Mavumbi ya nchi + Ubavu + Hawa + Bustani + Mti wa ujuzi wa mema na mabaya.
2. Tunda + Nyoka + Hautakufa + Uongo.
3. Twa tunda + Aibu + Adhabu + Laani nchi + Mavasi.
4. Kifo + Mwokozi + Tii Mungu.

**2.1** Mungu aliumba Adamu kutoka kwa mavumbi ya nchi. Alichukuwa ubavu wa Adamu na akamtengezea mke. Adamu alimuita Hawa.

Mungu alitengenezea Adamu na Hawa bustani nzuri ya kuishi, na kila aina ya matunda na maua ya kupendeza. Walikuwa na kila kitu walichohitaji.

“Tunda la kila mti wa bustani waweza kula”, Mungu alisema.

Lakini kulikuwa na kitu kimoja tu, Mungu alisema wasifanye. Kitu kimoja tu. Katikati ya bustani kulikuwa na mti ulioitwa mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

“Sharti (Lazima) usile tunda lake, la sivyo utakufa,” Mungu alisema.

**2.2** Adamu na Hawa walikuwa na furaha katika Bustani ya Edeni. Lakini Hawa alizoea kwenda kuangalia huo mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Tunda lake lilipendeza.

Wakati moja alipokuwa akiangalia, nyoka akamuzungumzia.

“Eti Mungu amesema msile tunda la huu mti?” akamuuliza.

“Mungu ametwaambia tukila tunda la mti huu tutakufa,” Hawa akajibu.

Nyoka akasema, “Hamtakufa. Mungu amejua mkila tunda lake mtakuwa kama yeye, mtajua mema na mabaya”

Hapa kuna uongo wa kwanza ulioleta taabu nyingi baadaye.

**2.3** Hawa alitwaa tunda kutoka kwa huo mti na akala, akampa Adamu pia akala.



Waliaibika baada ya kula hilo tunda, kwa maana kwa mara ya kwanza wakajiona wako uchi. Walijaribu kujificha kwa kujitengenezea mavasi ya majani.

Waliposikia Mungu akiwaita, walijificha.

Mungu akawauliza, “Mmekula kwa huo mti niliowakataza msile?”

Adamu akalaumu Hawa, na Hawa akalaumu nyoka. Lakini Hawa angemtii Mungu kwa kutosikiliza nyoka.

Mungu akawaadhibu kwa kutomutii.

Nyoka alitambaa kwa tumbo na kula mavumbi.

Mwanamke awe na watoto wengi.

Adamu afanye kazi ya jasho ili wapate chakula wale, kwa maana Mungu alilaani nchi.

Mungu aliwapa mavasi kutoka kwa ngozi ya wanyama.

**2.4** Adhabu mbaya saidi ilikuwa kifo. Wote wawili, Adamu na Hawa watakuwa wazee na wafe vile Mungu alikuwa amewambia.

Angalau Mungu aliwaadhibu Adamu na Hawa, aliwapa tumaini kwa maana aliwaaidi siku moja watapata mwokozi awaokoe kutoka kwa kifo na kishinda madhara yaliyoletwa na uongo wa nyoka.

Huyo mwokozi ni Bwana Yesu Kristo anayetuokoa kutoka kwa dhambi zetu, tukimwamini na kutenda vile anatuambia.

Tunajifunza masomo mengi sana kutoka kwa Adamu na Hawa. La muhimu tujaribu kumtii Mungu na tuiseme uongo.